# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Nkoani,
S.L.P 273,
55103 RUKWA,
Barua pepe: rbcrukwa@pccb.go.tz.
TANZANIA.

## TAKUKURU RUKWA YASHINDA KESI

**Ndugu Wanahabari,**

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Machi, 2022, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007 kupitia madawati ya Uchunguzi na Mashtaka, Uzuiaji Rushwa pamoja na Elimu kwa Umma.

### UCHUNGUZI NA MASHTAKA

**(i) Taarifa zilizopokelewa (Kisekta).**

Katika kipindi hiki, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa imepokea jumla ya **taarifa 63.** Kati ya hizo, **taarifa 46** zilihusu rushwa na **taarifa 17** hazikuhusu rushwa. Katika taarifa 46 zinazohusu Rushwa na kuanzishwa uchunguzi wa awali (*Preliminary Investigation*), taarifa 14 zilifunguliwa majalada na kufikia hatua mbalimbali za uchunguzi kamili na jalada moja (01) kukamilika na watuhumiwa tayari wamefikishwa Mahakamani. Taarifa 32 bado zinaendelea na uchunguzi wa awali. Aidha taarifa 17 ambazo hazihusiani na Rushwa ofisi imetoa ushauri kwa watoa taarifa na kuwaelekeza mahali sahihi pa kuwasilisha malalamiko hayo. Hakukuwa na taarifa iliyohamishiwa idara nyingine. Taarifa hizi zimepokelewa kisekta kwa mchanganuo ufuatao:-

| DARA/SEKTA | SUMBAWANGA | KALAMBO | NKASI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| TAMISEMI | 8 | 6 | 3 | 17 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| BINAFSI | 7 | 4 | 2 | 13 |
| AFYA | 1 | 0 | 4 | 5 |
| POLISI | 1 | 2 | 1 | 4 |
| KILIMO | 0 | 0 | 1 | 1 |
| TRA | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Mahakama | 2 | 0 | 0 | 2 |
| Siasa | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Serikali Kuu | 1 | 1 | 0 | 2 |
| **JUMLA KUU** | **20** | **15** | **11** | **46** |

**(i) Kesi zilizoendelea Mahakamani.**

Katika kipindi hiki, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa ilikuwa na jumla ya **kesi nane (08)** zilizokuwa zikiendelea mahakamani. Pia katika kipindi hicho **kesi moja (01)** ilifunguliwa Mahakamani na kufanya kuwa na jumla ya **kesi tisa (09)** zilizokuwa zikiendeshwa katika Mahakama mbalimbali za Mkoa wa Rukwa.

Kati ya kesi hizo tisa (09) jumla ya **kesi mbili ziliamuliwa** ambapo Jamhuri ilishinda kesi moja (1) na kushindwa kesi moja (1).

**UZUIAJI RUSHWA**

**Ndugu Wanahabari,**

Ili kuboresha mifumo mbalimbali ya utoaji wa huduma kwa wananchi, katika kipindi hiki TAKUKURU Mkoa wa Rukwa iliendelea kufanya chambuzi mbalimbali za **mifumo mitatu** ikiwemo Mfumo wa utendaji kazi wa wakala wa huduma za ufundi na umeme (TEMESA) katika tathmini ya utoaji wa huduma za matengenezo ya magari, Uchambuzi wa mfumo wa Usimamizi wa mapato yanayotokana na ushuru wa madini ya ujenzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo pamoja na Utafiti mdogo wa kubaini vitendo vya Rushwa ya ngono katika idara ya elimu Wilaya ya Nkasi.

Aidha tumefanya ufuatiliaji wa miradi **ishirini na nne (24)** yenye jumla ya thamani ya **sh. 5,096,582,076/=**ili kujua kama kweli fedha iliyotumika inalingana na kazi iliyofanyika**.** Katika ufuatiliaji huu mianya iliyobainishwa ambayo ingeweza kusababisha rushwa, ilishauriwa namna bora ya kuiziba na Miradi Kuendelea na Ujenzi.

Ufuatiliaji wa wadaiwa (*Defaulters*) wa ukusanyaji mapato (*POS*) unaendelea katika Halmashauri zote za Mkoa wa Rukwa ili kuhakikisha fedha wanazodaiwa zinarejeshwa.

**TAARIFA YA MIRADI ILYOTEMBELEWA**

| S/N | JINA LA MRADI | THAMANI |
|---|---|---|
| 1. | Mradi wa uboreshaji na upandishaji wa hadhi ya barabara ya Miangalua - Movu 8km kuwa ya Changarawe na Miangalua – Chombe - Kipeta 10km kuwa ya changarawe katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa | 479,307,500.00 |
| 2. | Mradi wa ukarabati wa barabara ya Lusaka-Lowe-Laela 19.3 km katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa. | 471,364,000.00 |
| 3. | Mradi wa upandisaji wa hadhi 7.5 km wa barabara ya Kilyamatundu -Ilambo kuwa ya Changarawe katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa. | 167,460,000.00 |
| 4. | Mradi wa upandisaji wa hadhi 8.1km wa barabara ya Mpui-Kapewa - Mpwapwa kuwa ya changarawe katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa. | 187,305,000.00 |
| 5. | Mradi wa ujenzi wa Box Kalavati moja katika barabara ya Kamita – Mnadani, ujenzi wa mfereji 300m katika barabara ya Mtumbuka na mfereji 200m barabara ya Sumbawanga Asilia - Katusa katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga Asilia Mkoa wa Rukwa. | 99,436,330.00 |
| 6. | Mradi wa matengenezo ya sehemu korofi katika barabara ya Katumba Azimio – Pito – Malagano 2km, Mlanda–Pito 2km, ujenzi wa mfereji 400m katika barabara ya Mlanda A – Mlanda B, matengenezo ya | 110,822,400.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | kawaida barabara ya Malonje – Molo –Gerezani 3.3 na barabara ya Katumba Azimio–Malonje 5km katika halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa. | |
| 7 | Mradi wa matengenezo ya sehemu korofi katika barabara ya Special 0.4km, Nyami 1.2km, Airport – Senga–Wipanga 2km, matengenezo maalumu barabara ya Regional Block – Msakila 1km, matengenezo ya kawaida barabara ya Special 3km, Sumbawanga Asilia – Kankwale 2km na Kankwale – Luwa 6km katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa. | 127,803,800.00 |
| 8 | Mradi wa matengenezo maalumu ya barabara ya Kristo Mfalme – Kati 1km, Majengo – Mponda 1.5km, matengenezo ya sehemu korofi katika barabara ya Kisiwani – King'ombe – Mawenzusi 1km, Malichewe 1km, matengenezo ya kawaida barabara za Mbizi Hotel – Kristo Mfalme 1km, Mwaiseni –Johnkela –King'ombe 2.5km, Isesa – Nambogo 3.9km katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa. | 157,297,430.00 |
| 9 | Mradi wa ujenzi wa box Kalavati na ukarabati wa daraja moja barabara ya Kizwite – Chelenganya, matengenezo ya sehemu korofi katika barabara ya Kisumba – Chelenganya 1km, matengenezo ya kawaida barabara ya Machinjio – Malangali 2.5km na barabara ya Kasesya – Redio Chemchem 1km katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa. | 135,785,616.00 |
| 10 | Mradi wa ujezi wa daraja na barabara ya Kasitu – Jengeni km 10 na barabara vya Mambwekenya - Madibira km 5 (pesa za mfuko wa jimbo) Wilaya ya Kalambo | 500,000,000/ |
| 11 | Mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Mwazye Wilaya ya | 500,000,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | Kalambo | |
| 12 | Mradi wa ujenzi wa madarasa 5 ya shule ya sekondari ya Msanzi fedha za UVIKO 19 Wilaya ya Kalambo | 100,000,000/= |
| 13 | Mradi wa ujenzi wa madarasa 5 ya shule ya sekondari Kalambo fedha za UVIKO 19 Wilaya ya Kalambo | 100,000,000/ |
| 14 | Mradi wa ujenzi wa madarasa 4 ya shule ya sekondari Kanyele fedha za UVIKO 19 Wilaya ya Kalambo | 80,000,000/ |
| 15 | Mradi wa ujenzi wa madarasa 3 ya shule ya sekondari Machinda fedha za UVIKO 19 Wilaya ya Kalambo | 60,000,000/ |
| 16 | Mradi wa ujenzi wa madarasa 3 ya shule ya sekondari Katazi fedha za UVIKO 19 Wilaya ya Kalambo | 60,000,000/ |
| 17 | Mradi wa ujenzi wa madarasa 3 ya shule ya sekondari Mwazye fedha za UVIKO 19 Wilaya ya Kalambo | 60,000,000/ |
| 18 | Mradi wa ujenzi wa madarasa 4 ya shule ya sekondari Namema fedha za UVIKO 19 Wilaya ya Kalambo | 80,000,000/ |
| 19 | Mradi wa ujenzi wa madarasa 4 ya shule ya sekondari Isenga fedha za UVIKO 19 Wilaya ya Kalambo | 80,000,000/ |
| 20 | Mradi wa ujenzi wa madarasa 4 ya shule ya sekondari Matai fedha za UVIKO 19 Wilaya ya Kalambo | 80,000,000/ |
| 21 | Ukarabati barabara ya Kasu Mpimbwe Wilaya ya Nkasi | 300,000,000 |
| 22 | Ujenzi wa Jengo la dharura na nyumba 2 za watumishi Hospital ya Wilaya Nkasi | 390,000,000 |
| 23 | Ujenzi wa Shule ya Sekondari na Kata ya Paramawe Wilaya ya Nkasi | 470,000,000/= |
| 24 | Ukarabati barabara ya Kasu Mpimbwe Wilaya ya Nkasi | 300,000,000 |
| **JUMLA KUU** | | **5,096,582,076/=** |

Katika zoezi la kufuatilia miradi hii ilibainika kuwa, baadhi ya barabara zilizojengwa na zinazoendelea kujengwa na Wakandarasi, hazijawekwa alama za barabarani na mifereji ya maji kwa kadri ilivyo kusudiwa na pia kumekuwa na ucheleweshwaji wa kuikamilisha miradi hiyo. Ili kurekebisha kasoro hizo,

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa imetoa ushauri kwa Wakandarasi wanaoendelea na ujenzi wa barabara na madarasa, kukamilisha miradi hiyo kwa wakati ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria pindi watakapo shindwa kukamilisha miradi hiyo kwa wakati kwa mujibu wa mikataba.

**ELIMU KWA UMMA**

**Ndugu Wanahabari,**
Katika kuhakikisha kwamba Wananchi wa Rika na Kada mbalimbali katika Mkoa wa Rukwa wanaendelea kupewa elimu na uelewa juu ya vitendo vya Rushwa ili washiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya Rushwa ndani ya jamii yetu, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa imefanya jumla ya semina kumi na sita (16), imeimarisha Klabu za Wapinga Rushwa kumi na moja (11) katika Shule za Sekondari kwa lengo la kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa na kuwajenga wanafunzi kimaadili.

**USHIRIKIANO WA TAKUKURU NA SKAUTI (TAKUSKA)**:

Vilevile, katika kipindi hiki, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa kwa kushirikiana na Makamishna wa Skauti wa Wilaya na Mkoa imefanya semina saba (7) kwa ajili ya kuendelea kuutambulisha Mwongozo wa Mafunzo kwa Wawezeshaji wa Kufundishia Vijana wa Skauti Kuhusu Kuzuia na Kupambana na Rushwa ngazi ya Kata na Tarafa kwa lengo la kuwajenga vijana wa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo katika misingi ya Uzalendo, Uwajibikaji na kutojihusisha na Vitendo vya Rushwa.

Aidha, katika kipindi hiki TAKUKURU Mkoa wa Rukwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo baadhi ya Wakuu wa Idara katika Halmashauri za Wilaya, Maafisa Watendaji wa Kata, Mitaa na vijiji, Maafisa Tarafa, Waheshimiwa Madiwani, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Wakuu wa Vituo vya Polisi wakiwemo Watumishi wa Serikali za Mitaa katika maeneo husika kufanya mikutano ya hadhara saba (7) ikiwemo mitatu (3) kupitia *"PROGRAMU YA TAKUKURU INAYOTEMBEA (PCCB MOBILE)"* kwa lengo la kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi katika maeneo yao;

imerusha vipindi vya redio vinne (4), imeandika makala tano (5), imeshiriki katika wiki ya sheria pamoja na kuongea na Waandishi wa Habari ili kuhakikisha elimu ya mapambano dhidi ya rushwa inawafikia wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa na maeneo mengine ya Tanzania.

**MIKAKATI YA MWEZI APRILI HADI JUNI, 2022:**

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa kupitia Dawati la Uzuaji Rushwa itaendelea kufanya ufuatiliaji wa fedha zinazotolewa na Serikali katika ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo na ile ya UVICO – 19 inayoendelea kutekelezwa katika Halmashauri za Wilaya kwa lengo la kuziba mianya ya rushwa na kudhibiti upoteaji wa fedha za serikali katika utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kufuatilia Miradi ya Ujenzi wa barabara zilizo chini ya TARURA.

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa itaendelea pia kufanya udhibiti na uchunguzi kuhusu ubadhirifu wa fedha za serikali katika ugavi wa dawa na bidhaa za afya (vifaa tiba) ambao umekuwa ukijitokeza katika Vituo vya Afya na Hospitali za Serikali Mkoa wa Rukwa ili wote wanaohusika na ubadhirifu huo wachukuliwe hatua za kisheria. Aidha, kwa upande wa Uelimishaji Umma tutaendelea na uelimishaji huku msisitizo mkubwa ukiwa katika kuendeleza ushirikiano kupitia TAKUKURU na SKAUTI kwa kuwalenga vijana.

Kwa upande wa Uchunguzi na Mashtaka, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa inakusudia kufikisha Majalada Manne (4) Ofisi ya Mashtaka ili kupata Vibali vya kuyafikisha Mahakamani.

**WITO:**

**Ndugu Wanahabari,**

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa bado inaendelea kutoa rai kwa wale wote wanao watapeli wananchi kwa kujifanya maafisa wa TAKUKURU na wale wanaoendelea kujihusisha na vitendo vya rushwa waache mara moja, kwani wakikamatwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa tunaendelea kutoa shukrani kwa viongozi mbalimbali na wanannchi kwa kuendelea kuunga mkono mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa zinazohusu vitendo vya rushwa.

Aidha, TAKUKURU tunawashukuru sana wana habari wote katika Mkoa wetu wa Rukwa ambao mmekuwa mstari wa mbele kufikisha elimu hii ya mapambano dhidi ya rushwa kwa wananchi wa mkoa wa Rukwa na maeneo mengine, maana jukumu la mapambano dhidi ya rushwa si la TAKUKURU pekee bali linamhusu kila mtu/mtanzania.

**Imetolewa na:**

**DANIEL NTERA**
**MKUU WA TAKUKURU (M) RUKWA**
**SIMU: 0738150186**